

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO



MWALIKO KWA WADAU WA KUSHIRIKI KATIKA SHUGHULI ZA KAMATI YA SERA ZA KODI (TASK FORCE ON TAX REFORM) KWA AJILI YA MATAYARISHO YA BAJETI YA 2018/19

Kamati ya Ushauri ya Sera za Kodi (Task Force on Tax Reform) kwa ajili ya matayarisho ya Bajeti ya Serikali 2018/19 itaanza kazi yake mnamo mwezi Februari 2018. Sekretariati ya Kamati inaandaa mkutano wa wadau, kwa ajili ya kuwasilisha mada na kuzijadili. Serikali itaongoza mjadala kwa kutoa malengo yake ya sera, agenda, changamoto na kutathmini vipaumbele vya sera za mapato katika bajeti ya 2018/19. Hali hii itawapa washiriki mtazamo mpana zaidi kuhusiana na shughuli za mwaka huu na kuhamasisha uchambuzi na majadiliano ya mapendekezo mbalimbali kwa undani zaidi.

Sera za mapato zinalenga kupanua wigo wa kodi, kuboresha zaidi mfumo wa kodi na taratibu za ukusanyaji, kuongeza ufanisi wa ukusanyaji na uhibitaji ukwepaji wa kodi. Aidha, lengo kuu la Serikali ni kuweka mfumo wa kodi wenye kuboresha mazingira ya uwekezaji na uzalishaji ili kukuza uchumi.

Kamati inakaribisha ushiriki wa Maafisa wa Serikali, Sekta Binafsi, Asasi Zisizo za Serikali, Taasisi za Dini, jamii ya wasomi, taasisi za utafiti na wataalam wengine katika sekta ya uchumi. Vile vile, Kamati inakaribisha mada mbalimbali kwa maandishi kutoka kwa wale wanaopenda kufanya hivyo. Mada hizo hazina budi kuonyesha yafuatayo:-

- Mtu, Kampuni/makampuni, taasisi au chama/vyama ambavyo wanawakilisha;
- Mapendekezo ya mabadiliko katika mapato ya serikali yanayotokana na kodi na yasiyo ya kodi, ikiwa ni pamoja na uchambuzi wa sekta, maeneo au aina ya walipa kodi ambao wataathirika, na kwa namna gani;
- Makisio ya athari kwenye uchumi na mapato ya serikali katika mwaka huu wa utekelezaji na katika miaka ijayo.
- Sababu na uhalali wa mapendekezo ya mabadiliko kwenye sera za mapato na hususan uchambuzi wa namna ambavyo mapendekezo hayo yataisaidia Serikali kufanikisha malengo yake makuu ya kiuchumi, kodi na kupunguza umasikini.
- Pale ambapo mapendekezo yanapunguza mapato ya Serikali (hata katika kipindi cha muda mfupi), mapendekezo hayo hayana budi yaweke hatua bayana na za kuaminika sambamba na msukumo wa jumla wa sera za bajeti ya Serikali ili kufidia upungufu wa mapato ambao utajitokeza.

Kamati ya Ushauri wa Sera za Kodi kwa muda mrefu sasa imekuwa ikifanikisha majadiliano ya masuala mbalimbali yanayohusiana na sera za kodi na usimamizi wake. Mikutano hii imekuwa ikitoa mchango mkubwa kwa waandaa sera (policy makers) kwa muda mrefu. Hali hii imesaidia sana katika kuunda mfumo wa kodi ambao kwa kupitia majadiliano/mazungumzo na uchambuzi umewezesha utatuzi wa masuala mbalimbali ya kodi kwa ufasaha na uwazi. Tunahitaji michango yenu ili kuendelea na majadiliano haya kati ya wadau katika masuala mbalimbali ya Uchumi.

Mwisho, mada zote na mapendekezo yawasilishwe kuanzia sasa hadi tarehe 10 Februari 2018 kwenye Sekretariati ya “Task Force on Tax Reform”, Wizara ya Fedha na Mipango, Idara ya Sera, Chumba Namba. 339 (Jengo Kuu la Hazina), Dar es Salaam.

Doto M. James
KATIBU MKUU HAZINA
Disemba,2017